

Nambari ya Mtahiniwa \_\_\_\_\_

**SMZ**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA DARASA LA NNE**

**121**

**KISWAHILI**

**MUDA : SAA 2.00**

**JUMATATU 20/11/2017, mchana**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

- 1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.**
- 2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Swali MOJA (1) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.**
- 3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
- 4. Jawabu zote ziandikwe ndani ya nafasi zilizowekwa.**

<b>KWA MATUMIZI YA USAHIHISHAJI</b>		
<b>NAMBARI YA SWALI</b>	<b>ALAMA</b>	<b>SAINI</b>
<b>1.</b>		
<b>2.</b>		
<b>3.</b>		
<b>4.</b>		
<b>5.</b>		
<b>6.</b>		
<b>7.</b>		
<b>8.</b>		
<b>9.</b>		
<b>10.</b>		
<b>JUMLA</b>		

**Mtihani huu una kurasa 8 zenye maandishi**

**SEHEMU A: (Alama 20)**

**UFAHAMU**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii**

Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

Mwalimu Jecha alitufundisha kuhusu ubaya wa ajira kwa watoto. Alisema kwamba Serikali imepiga marufuku ajira ya watoto. Kila siku inapiga mbiu lakini bado baadhi ya watu huwatumia watoto katika kazi kwa malipo kidogo. Mara nyingine huwafanyisha kazi bila kuwapa chohote. Kazi huwa ni nzito kuliko wanavyoweza kuzimudu, hivyo huhatarisha afya zao. Serikali imekula kiapo kuwaadhibu watu hao.

Mwalimu Jecha alisema, watoto hutumiwa katika biashara na kazi za ndani. Imekuwa kawaida kuwaona watoto wakifanya biashara za matunda, maji, kahawa na tangawizi.

Wakati mwengine watoto hawa huwa hawafanyi hivyo kwa kupenda. Shida ndio husababisha watoto kujikuta katika hali hiyo. Baadhi ya watoto ni mayatima. Wazazi wao wamefariki kwa ajali na magonjwa mbali mbali. Wengine huwa wametelekezwa na wazazi baada ya kutengana.

**1. Maswali**

i) Mwalimu Jecha alitufundisha kuhusu nini?

---

---

ii) Taja kazi mbili (2) wanazofanyishwa watoto.

---

---

iii) Ni jambo gani linalopelekea watoto kujikuta wakitumiwa katika ajira za watoto?

---

---

iv) Watoto wanaojikuta katika ajira ya watoto, wazazi wao mara nyingi huwa wapi?

---

---

v) Serikali imekula kiapo gani dhidi ya wanaowaajiri watoto?

---

---

2. Andika maana ya maneno yaliyopigiwa mstari.

i) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

ii) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

iii) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

iv) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

v) \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

**SEHEMU B: (Alama 40)**

**SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii**

3. Taja aina ya vielezi vilivyopigiwa mstari.

i) Halima amekwenda mtoni.

ii) Babu yake anatembea taratibu.

iii) Yule anakwenda wapi?

iv) Dada atafika kesho jioni.

v) Wanafunzi wamezunguka uwanja mara tatu.

4. Andika sentensi zifuatazo kwa uyakinifu.

Kwa mfano: Ali hali embe.

Ali anakula embe.

i) Watoto hawa hawapendi somo la Kiswahili.

ii) Mzee hafui nguo zake.

iii) Huu si mzigo wa mwisho.

iv) Nyimbo hazina faida.

v) Hili haliwekwi kesho.

5. a) Chagua neno kutoka **KUFUNGU A** linalowiana na **KIFUNGU B**. Andika herufi ya jawabu sahihi ndani ya mabano.

<b>KIFUNGU A</b>	<b>KIFUNGU B</b>
i. Mtama, mchele, Maharage, Kunde.(     )	
ii. Kitanda, Kabati, Meza, Viti. (     )	a. Chembechembe
iii. Samaki, dagaa, nyama ya ng'ombe nyama ya kuku. (     )	b. Nguo
iv. Mchicha, kisamvu, figili, mtoriro. (     )	c. Wanyama
v. Kanga, mtandio, buibui,kanzu. (     )	d. Mboga
	e. Nafaka
	f. Samani
	g. Kitoweo
	h. Thamani

- b) Andika maneno yafuatayo kwa nambari.

i) Elfu ishirini na mia sita

\_\_\_\_\_

ii) Laki tatu

\_\_\_\_\_

6. a) Andika nambari zifuatazo kwa maneno.

i) 2,500

\_\_\_\_\_

ii) 75,000

\_\_\_\_\_

iii) 450,000

\_\_\_\_\_

**Nambari ya Mtahiniwa \_\_\_\_\_**

b) Uliza maswali yafuatayo kwa lugha ya Kiswahili.

i) Who is the president of this country?

\_\_\_\_\_

ii) Where is Mnazi-mmoja hospital?

\_\_\_\_\_

**SEHEMU C: (Alama 20)**

**FASIHI**

**Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii**

7. Andika hadithi inayotufunza “Umuhimu wa Kuwaheshimu Wazazi”.

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

8. Andika maana za nahau zifuatazo.

i) Ana mkono wa buli.

\_\_\_\_\_

ii) Kujikaza kisabuni.

\_\_\_\_\_

iii) Kaa mkao wa kula.

\_\_\_\_\_

iv) Mezea mate.

\_\_\_\_\_

v) Kula chumvi.

\_\_\_\_\_

**SEHEMU D: (Alama 20)**

**UTUNGAJI**

**Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii**

9. Muandikie barua baba yako ambaye yuko Dar-es-Salaam umueleze kuhusu mtihani wako uliofanya.

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

10. Andika mambo matano (5) muhimu yanayopaswa kuandikwa katika kadi ya mwaliko.

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

-----